

# MTAALA MPYA WA UMILISI

GREDI YA 3, - MWAKA: 2021

## SHUGHULI ZA KISWAHILI

SASON  
002

Jina: \_\_\_\_\_

Nambari ya mwanafunzi:

Jinsia: Mvulana  Msichana

Jina la kaunti: \_\_\_\_\_ Nambari ya kaunti

Jina la kaunti ndogo: \_\_\_\_\_ Nambari ya kaunti ndogo

Jina la shule: \_\_\_\_\_ Nambari ya shule

Jedwali lifuatalo lijazwe baada ya mwalimu  
kusahihisha kazi ya mwanafunzi.

	Kiwango 1	Kiwango 2	Kiwango 3	Kiwango 4
Sehemu 1				
Sehemu 2				
Sehemu 3				
Sehemu 4				
Sehemu 5				

**SEHEMU 1: KUSIKILIZA NA KUONGEA**  
**Mwalimu amuulize mwanafunzi maswali yafuatayo.**

1. Habari yako?  
*(Mwanafunzi ajibu)*
2. Taja tunda unalolipenda.  
*(Mwanafunzi ajibu)*
3. Tunda hilo linapatikana wapi?  
*(Mwanafunzi ajibu)*
4. Kabla ya kula tunda unafaa ufanye nini?  
*(Mwanafunzi ajibu)*
5. Tunda hilo huwa tamu likiwa bivu au bichi?  
*(Mwanafunzi ajibu)*

**Vigezo vya Kutathminia - Kusikiliza na Kuongea**

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Upeo / Alama	5	4	3	0 - 2

**SEHEMU 2: KUSOMA KWA SAUTI**

Soma kifungu hiki kwa sauti.

Niliamka asubuhi na mapema. Kulikuwa na utulivu kwa sababu watu wengi hawakuwa wameamka. Hata wazazi wangu bado walikuwa wakilala. Nilienda bafuni nikaoga. Kisha nikaenda jikoni kutayarisha staffahi. Sikutaka nichelewe kufika shulen. Baada ya kupata staffahi, nilipiga meno mswaki kisha nikavaa sare za shule. Nilitoka mbio hadi shulen. Siku hiyo ilikuwa siku ya kuzuru mbuga ya wanyama.

**Vigezo vya Kutathminia - Kusoma kwa Sauti**

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Maneno yaliyosomwa katika dakika moja	46 na zaidi	31 - 45	16 - 30	0 - 15

**SEHEMU 3: UFAHAMU**

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.

Hapo zamani za kale, kuku na mwewe. Walikuwa marafiki wa chanda na pete. Walikuwa wakiishi pamoja. Kila asubuhi walienda kulima katika shamba lao. Kuku alikuwa na vifaranga watano naye mwewe alikuwa na makinda wawili.

Siku moja kuku alimkanyaga kinda mmoja hadi akaaga dunia. Ingawa ilikuwa ajali, mwewe aliapa kulipiza kisasi. Kuku aliamua kutoroka hadi kwa binadamu. Tangu siku hiyo, mwewe huwashika vifaranga wa kuku kulipiza kisasi.

1. Kila asubuhi kuku na mwewe walienda wapi?
2. Kuku alikuwa na vifaranga wangapi?
3. Mwewe alikuwa na makinda wangapi?

4. Nani alimkanyaga kinda?  
 5. Kuku alitoroka hadi wapi?

**Mwongozo wa Kutathminia - Ufahamu**

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Upeo / Alama	5	4	3	0 - 2

**SEHEMU 4: SARUFI**

Kanusha sentensi.

1. Enda nyumbani.  
 2. Mtoto anakula ndizi.  
 3. Baba analima shambani.  
 4. Kaka amepika chakula.  
 5. Soma kitabu hiki.

Andika kinyume.


6. Shuka - 9. Funika -  
 7. Rudi - 10. Jenga -  
 8. Keti -

Andika tarakimu kwa maneno.


11. 86 -  
 12. 92 -  
 13. 126 -  
 14. 74 -  
 15. 225 -

Andika majina ya maumbo haya.


16. 17. 18.



- 19.



- 20.



Andika manenc kwa wingi.

21. Uzi -  
 22. Ukuta -  
 23. Meza -  
 24. Tunda -  
 25. Mwanafunzi -

**Mwongozo wa Kutathminia - Sarufi**

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Upeo / Alama	22 - 25	15 - 21	8 - 14	0 - 7

## SEHEMU 5: KUANDIKA

INSHA

## Andika insha juu ya:

# DARASA LETU

## Mwongozo wa Kutathminia - Kuandika

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Upeo / Alama	10	7 - 9	4 - 6	0 - 3